SEPTEMBA 2022

Dart Jarida

Toleo la Mtandaoni.

# PIC yataka DART kuongeza Mtandao wa Barabara zake.

Wakati Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) ukiendelea kusimamia ujenzi, usanifu, na uendeshaji wa huduma ya usafiri wa umma mkoani Dar es Salaam, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) imeishauri Serikali kupitia Wakala huo kufanya upembuzi yakinifu wa mtandao wa barabara zake ili kuongeza njia nyingi zaidi hasa katika maeneo ambayo hayakua katika mipamgo yake kwani ukuaji wa mji unaenda kwa kasi sana.

Akizungumza wakati wa ziara ya Kamati hiyo kutembelea na kujionea maendeleo ya mradi huo mapema mwezi huu, Mwenyekiti wa Kamati ya PIC Mh.Jerry Silaa alisema upembuzi kuhusu miundombinu ya barabara za Mabasi Yaendayo Haraka ulifanyika mwaka 2004 kipindi ambacho maendeleo ya makazi pamoja na ongezeko la watu lilikua kidogo.

“Wakati upembuzi wa ujenzi wa barabara za Mabasi Yaendayo Haraka unafanyika miaka hiyo ya zamani Mkoa wa Dar es Salaam haukuwa na wakazi wengi, lakini pia haukua na maendeleo kama hivi sasa, hivyo serikali ione namna ya kuongeza mtandao wa barabara zenu ili kuwafikia wananchi wengi Zaidi” alisema mwenyekiti.

Alisema kasi ya ukuaji wa mji inaongeza wahitaji wa usafiri wa umma hivyo Wakala ujipange kusanifu barabara katika maeneo mengine, akitolea mfano barabara iliyosanifiwa kuishia Boko inaweza kuongezwa hadi Kerege ama Mapinga Bagamoyo, barabara ya Kilwa iishie vikindu na barabara ya Pugu iende hadi Pugu kwa ajili ya kuhudumia wakazi wa Chanika hadi Kisarawe.

Pia Kamati ilipendekeza DART kufikiria kupeleka huduma katika miji mikubwa kama Arusha,Mbeya, Mwanza, na Dodoma, ambako ndio Makao Makuu ya Serikali na kuna shughuli nyingi zinazohitaji uwepo wa Mabasi Yaendayo Haraka.

Kamati hiyo, iliupongeza Wakala kwa kuendelea kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato baada ya kuanza kutumika kwa mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa nauli.

“Niipongeze kwa dhati DART kwa jinsi mlivyoweza kuongeza ukusanyaji wa mapato kutoka Tsh.bilioni 25 hadi Tsh. Bilioni 36 katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2021/2022” Alisema Mh.Silaa.



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma **(PIC)**, Mhe. Jerry Silaa, akitoa maelekezo ya jinsi ya kuboresha mradi wa DART katika ziara ya kamati yake, iliyofanyika Septemba 2022.*

Kwa upande wake Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa alisema Wizara itaendelea kuisimamia na kuipa ushirikiano DART ili iweze kutimiza malengo yake ikiwemo kuiwezesha kimuundo.

“Mh.Rais ameridhia muundo mpya wa DART hivyo hii itawasaidia kuongeza ufanisi katika utendaji wenu wa kazi. Hii ni imani kubwa sana aliyonayo kwenu hivyo msimuangushe” Alisema Waziri Bashungwa.

Aidha, Waziri Bashungwa alisema Serikali iko katika hatua za mwisho za kusaini mkataba na mtoa huduma mpya ambaye ataleta mabasi 177 kwa ajili ya kuongeza wigo wa utoaji huduma kwa wakazi wa Dar es Salaam.

Mtendaji Mkuu wa DART Dr.Edwin Mhede alihakikishia kamati ya PIC kwamba Wakala umepokea mapendekezo ya kamati na kuahidi kuyafanyia kazi ili usafiri wa umma katika mkoa wa Dar es Salaam uwe wa kiwango cha kimataifa.

Mtandao wa barabara za DART unajumuisha Awamu ya kwanza yenye urefu wa kilometa 20.9 inayohusisha barabara ya Morogoro kuanzia Kimara hadi Kivukoni, barabara ya Kawawa eneo la Magomeni hadi Morocco , Msimbazi fire hadi Gerezani Kariakoo.

Awamu ya pili inahusisha barabara ya Kilwa kuanzia Gerezani hadi Mbagala Rangitatu, awamu ya tatu inahusisha barabara ya Nyerere kuanzia mjini kati hadi Gongolamboto, pamoja na awamu ya nne itakayojengwa katika barabara za Sam Nujoma na Ali Hassan Mwinyi.

Nyingine ni awamu ya tano katika barabara ya Nelson Mandela na Tabata dampo hadi Tabata Segerea, pamoja na awamu ya sita katika barabara ya Mwai Kibaki na nyongeza za Kimara hadi Kibamba Pamoja na Mbagala Rangitatu hadi Vikindu.

# Operesheni ya Kuzuia Magari Yanayovamia Barabara za BRT Yaendelea.

Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) unatekeleza operesheni maalum ya kuzuia magari yote ambayo yanapita katika barabara maalum kwa ajili ya Mabasi Yaendayo Haraka maarufu kama Mwendokasi, baada ya kukithiri kwa muingiliano kati ya magari binafsi, magari ya taasisi za umma na mabasi ambayo ndiyo pekee yanatakiwa kupita katika barabara hizo.

Kutekelezwa kwa operesheni hiyo kumekuja kutokana na kukithiri kwa watumiaji wa barabara hizo ambao kisheria hawatakiwi kutumia barabara za Mabasi Yaendayo Haraka.



*Maafisa wa Kikosi Kazi cha **DART** wakitekeleza majukumu yao ya kuzuia magari yanayovamia barabara za Mabasi Yaendayo Haraka.*

Zoezi hilo ambalo kwa kiasi kikubwa limeleta mafanikio makubwa kwa kupunguza idadi ya magari yanayovamia mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka limewaibua wakazi wengi wa Dar es Salaam kutoa maoni yao juu ya operesheni hiyo ambayo wameielezea kuwa yenye mafanikio makubwa.

Akizungumza katika Kituo cha Mwembechai moja ya vituo ambavyo operesheni hiyo inafanyika Abdul Mateso mkazi wa Magomeni amesema zoezi hilo ni muhimu kwani linazuia magari yasiyohusika na kuacha Mabasi pekee ndio yatumie miundombinu hiyo.

"Nimeshangaa kuona magari ya majeshi yakizuiwa kupita katika barabara za mwendokasi, zamani tuliona barabara hizi zikiwa zimejaa magari ya vyombo vya ulizini na usalama wakati mwingine hata watu binafsi wanajiamulia wanapita tu bila uoga, sasahivi nawaona DART wameamua kulivalia njuga suala hili, hii safi sana tunataka watu wote watii sheria bila kujali vyeo vyao wala taasisi wanazotoka" Alisema Mateso.

Zoezi la kuondoa magari na vyombo vingine vya moto katika barabara za Mabasi Yaendayo Haraka limenza katikati ya mwezi Septemba na linasimamiwa na Maafisa wa DART kwa kushirikiana na Kampuni ya ulinzi ya China Security Tanzania ambao ndio wenye dhamana ya kusimamia ulinzi na usalama katika miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka.
Wakati zoezi hilo likiendelea Jeshi la Polisi lilitoa tamko la katazo la magari ambayo sio mabasi kutumia barabara hizo na kusisitiza kufuatwa kwa sheria za matumizi ya barabara za Mabasi Yaendayo Haraka, na iwapo kutakuwa na ulazima wa gari ambalo sio Basi liendalo haraka kupita katika njia hizo ni lazima kuwe na kibali maalum ambacho kimetolewa na DART.

Taarifa hiyo ilisisitiza kuwa, barabara hizo zimejengwa kwa ajili ya Mabasi Yaendayo Haraka na si magari mengine hivyo kwa waliokua na mazoea ya kutumia barabara hizo kuacha mara moja kwani Kwenda ama kurudi kazini sio suala la dharura.

Katika utekelezaji wa operesheni hiyo zaidi ya magari 250 yalizuiliwa na kurudishwa yalikotoka kwa kipindi cha siku mbili za mwanzo mengi yakiwa ya serikali na vyombo vya ulinzi na usalama jambo ambalo linatatiza uendeshaji wa mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka.

Kwa upande wake Desdery Kawovela, mkazi wa Kimara Dar es Salaam amesema kwa kuwa muingiliano wa Magari ya Serikali katika Mfumo wa DART ni mkubwa ni vyema Serikali ikaamua kubadilisha matumizi ili barabara hizo zitumiwe na magari ya Serikali badala ya Mabasi.

"Haileti afya kabisa kwa mradi mkubwa wa kimkakati kama huu uliojengwa kwa mabilioni ya fedha ukachezewa kiasi hiki, mimi rai yangu kama magari ya Serikali ndio yanaonekana ya maana zaidi ya Mabasi, ikiwezekana wauue mradi huu ili barabara zipitwe na wao tu" Alisema Bw. Kawovela.

Kwa mujibu wa sheria zilizoanzisha Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka miundombinu ya barabara zake ni mahsusi kwa ajili ya Mabasi tu na si vinginevyo, na endapo kutakuwa na dharura ya aina yoyote itakayolazimu gari nyingine tofauti na Mabasi kutumia barabara hizo ni lazima kuwe na kibali maalum kutoka DART.

> "
> *Nimeshangaa kuona magari ya majeshi yakizuiwa kupita katika barabara za mwendokasi, zamani tuliona barabara hizi zikiwa zimejaa magari ya vyombo vya ulizini na usalama wakati mwingine hata watu binafsi wanajiamulia wanapita tu bila uoga, sasahivi nawaona DART wameamua kulivalia njuga suala hili, hii safi sana tunataka watu wote watii sheria bila kujali vyeo vyao wala taasisi wanazotoka*

# Umuhimu wa Mabasi Yaendayo Haraka.

Serikali yoyote makini na ambayo inawajali wananchi wake mara nyingi imekuwa ikijitahidi kutatua na kuondoa kero ili wananachi hao waishi kwa raha na kujivunia matunda ya uhuru wao. Hii imepelekea Serikali ya Jamhuri ya Muungano waTanzania kuanzisha mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka-BRT Jijini Dar es Salaam, au kwa jina maarufu kama Mabasi ya Mwendokasi yanayosimamiwa na Wakala wa DART, hii ilitokana na wananchi kuongezeka kwa kasi katika Jiji la Dar es Salaam hivyo kukawa na ulazima wa kuboresha miundombinu ya barabara pamoja na kupata mfumo mbadala wa usafiri mijini kwa ajili ya kupunguza msongamano wa magari pamoja na kurahisisha maisha kwa ujumla.



*Abiria wa Mabasi Yaendayo Haraka, wakisubiri kupata huduma katika kituo kikuu cha Kimara.*

Umuhimu wa mradi huu sio tu kwa wananachi wa Mkoa wa Dar es Salaam, bali hata kwa wageni wanaoingia katika Jiji na hata wale waishio katika maeneo ya mikoa ya jirani na Dar es Salaam.
Hii inatokana na ukweli kwamba Mabasi ya Mwendokasi yamerahisisha huduma ya usafiri kwakua yana uwezo wa kusafirisha watu wengi kwa wakati mmoja na wanafika wanakoelekea kwa muda mfupi sana kuliko ilivyokuwa awali wakati wa matumizi ya magari madogo madogo maarufu kama Daladala.

Pia mradi huu umekuwa kivutio kikubwa cha watalii kutoka maeneo mbalimbali barani Afrika na kwingineko ulimwenguni kwani wadau wengi wamekuja kujifunza jinsi unavyoendeshwa kwa minajili ya kwenda kuanzisha katika nchi zao hasa kwa nchi za Afrika.

Kwa mujibu wa usanifu wa miundombinu ya mradi wa DART utekelezaji wa mradi huo umegawanyika katika awamu Sita ambapo katika Barabara ya Morogoro ni Awanu ya kwanza inayofanya kazi kwa kipindi cha mpito kuanzia Kimara hadi Kivukoni na matawi yake ya Magomeni hadi Morocco, na katika barabara ya Msimbazi kuanzia Fire hadi Gezerani Kariakoo pamoja na kutokea eneo la Fire hadi Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.
Kuanza kwa mradi huo ambako kulifikiriwa na wengi kama ndoto za mchana kumewawezesha wasafiri kusafiri kwa muda mfupi zaidi kuliko ilivyokuwa awali maana kwa wastani mtu anaweza kutoka Kimara hadi Kivukoni kwa kutumia dakika 30 hadi 45 pekee jambo ambalo zamani lilikua haliwezekani ambapo wasafiri walitumia saa mbili hadi tatu kwa umbali huohuo.
Wale ambao wameonja uzuri na urahisi wa matumizi ya Mabasi Yaendayo Haraka watakubaliana na mimi kwamba, mfumo huu sio tu umerahisisha maisha ya wasafiri katika baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Dar es Salaam bali umepunguza gharama za mafuta kwa wale ambao wameamua kuacha magari yao binafsi na kutumia Mabasi hayo.

Umuhimu wa matumizi ya usafiri huu pia unaonekana kwa wanafunzi wa shule mbalimbali ambao wanautumia kwa unafuu na urahisi wa kuwahi shuleni asubuhi pamoja na kuwahi nyumbani wanaporejea wakati wa jioni, pia wanafunzi hawapati bugudha na unyanyasaji kama walipokuwa wanatumia usafiri wa Daladala.

Japokuwa bado kuna changamoto kadhaa katika uendeshaji wa mradi huu, ikiwemo ile ya uchache wa Mabasi pamoja na uchakavu wa Mabasi kadhalika ajali za mara kwa mara pamoja na muingiliano wa magari binafsi katika barabara za Mabasi Yaendayo Haraka, usafiri huo bado una faida lukuki kwa wananchi.

Kwa kutambua umuhimu na unyeti wa mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka DART, Serikali kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI ambao ndio wasimamizi wa mradi wanahangaika usiku na mchana kuhakikisha kero zilizopo katika mradi zinamalizika ili wanancnhi waendelee kufaidi matunda ya miradi mikubwa ya kimkakati ambayo inaibuliwa kwa ajili ya kuwapunguzia kero mbalimbali.

Hivi karibuni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa TAMISEMI Innocent Bashungwa alipotembelea Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka, Pamoja na kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mitaji ya Umma PIC alisema Serikali kupitia Wakala tayari inakamilisha hatua za mwisho za kumpata mtoa huduma ya mabasi ambaye ataagiza mabasi 177 kwa ajili ya kuongeza nguvu kwenye mfumo wa DART awamu ya kwanza.
Aidha Waziri Bashungwa alisema kuongezeka kwa idadi hiyo ya mabasi kutafanya mfumo wa awamu ya kwanza kuwa na idadi ya mabasi 305 ambayo ndiyo yanahitajika kwa mujibu wa usanifu wa mradi.

Kumalizika kwa baaadhi ya mradi wa DART kutasaidia kuimarisha usafiri wa umma katika mkoa wa Dar es Salaam na mikoa ya jirani kwani mahitaji ya usafiri wa umma ni makubwa hasa katika kusaidia ukuaji wa uchumi pamoja na kuimarisha upatikanaji wa mapato ya serikali.

Sambamba na maboresho katika uendeshaji wa mradi huo, ujenzi wa mioundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka katika barabara ya Kilwa kuelekea Mbagala unaendelea, kadhalika Mkandarasi kwa ajili ya kujenga awamu ya tatu ya mradi katika barabara ya Nyerere kuelekea Gongolamboto ameshakabidhiwa eneo la kazi ili aanze, Ni wazi Serikali imedhamiria kumaliza kabisa kero ya foleni mkoani Dar es Salaam.

Ukamilifu wa miundombinu ya DART kwa Awamu zote sita kutafanya Dar es Salaam kuwa miongoni mwa miji michache barani Afrika ambayo imefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika sekta ya usafiri wa umma.
Kuna usemi wa Kiswahili usemao mnyonge myongeni lakini haki yake mpeni, hivyo pamoja na changamoto zilizopo katika Mabasi Yaendayo Haraka bado yamekua mkombozi wa watanzania wengi ambao wanategemea usafiri wa umma katika shughuli zao za kila siku.

Wakati Serikali inaendelea kutatua changamoto zilizopo katika mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka, ni vyema wananchi kuvuta subra na kuendelea kumuunga mkono Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh.Samia Suluhu Hassan katika nia yake njema ya kuondoa kero ya usafiri wa umma mijini.

# Mamlaka ya barabara za Mijini Kenya KURA yatembelea DART.



*Wajumbe wa Mamlaka ya Barabara za Mijini kutoka nchini Kenya (KURA), wakipatiwa maelezo ya mfumo mpya wa ukusaji wa nauli, AFCS, Septemba 2022.*

Wajumbe kutoka Mamlaka ya barabara za mijini nchini Kenya KURA wamefanya ziara Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka kujifunza namna ambavyo mradi huo unaendeshwa, usanifu wake, pamoja na uendeshwaji wake ili wakaanzishe mradi wa namna hiyo nchini kwao.

Akizungumza katika ofisi za Wakala Ubungo Maji Dar es Salaam, kiongozi wa msafara huo Mhandisi Jancinta Mwangi alisema wameamua kuja kujifunza namna ya uendeshaji, miundombinu Pamoja na kujua changamoto zilizopo ili ziwasaidie katika kutekeleza azma yao ya kuanzisha mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka nchini Kenya.

“Katika ukanda wetu wa Afrika Mashariki Tanzania pekee ndio mna mradi wa namna hii ambao unaenda vizuri, sio tu kwenda vizuri lakini unapendezesha mandhari ya mji, hivyo tukaona ni vyema tuje ili kujifunza kwani kujifunza kitu kizuri kwa mtu aliyefanikiwa sio dhambi” Alisema Mhandisi Mwangi.

Alisema kwa namna ambavyo Kenya imejipanga wanataka kuanzisha mradi huo mara moja ili kuwapunguzia changamoto za usafiri wa umma hasa katika Jiji la Nairobi ambalo kero ya usafiri wa umma ni kubwa.


Katika msafara huo wajumbe hao wa KURA waliambatana na wataalam washauri wa miradi ya ujenzi kutoka nchini Kenya ambao ni Kampuni ya CAS Consultant sambamba na wale wa kampuni ya Kunhwa Engineering kutoka Korea ya Kusini ambao ndio wanatarajia kuwatumia katika kuandaa na kutekeleza mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka.

Ujumbe wa wataalam hao kutoka Kenya ambao ulifanya ziara yao kwa siku mbili, uliwasilishiwa mada mahsusi na wataalam wa DART kuhusu namna mradi ulivyoanza changamoto zilizopo, mapungufu pamoja na fursa ambazo zinatokana na uwepo wa mradi mkubwa wa kimkakati kama huo.
Aidha ujumbe huo ulitembelea na kujionea maendeleo ya ujenzi wa mradi wa BRT Awamu ya Pili kuelekea Mbagala katika vituo vikuu vya Gerezani, Mbagala Rangitatu Pamoja na vituo mlishi vilivyokamilika katika ushoroba huo.

Kwa upande wake Mhandisi Mohamed Kuganda kutoka DART alisema ufanisi wa uendeshaji wa mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam ndio unawavutia wageni mbalimbali kuja kujifunza.
“Mradi huu ni wa kipekee na kwakuwa viwango vilivyotumika ni vya kimataifa wageni wengi wamekua wakija kujifunza kwa lengo la kuona namna unavyoendeshwa ili wakaanzishe katika nchi zao, na hii sio mara ya kwanza tunapokea wageni wa namna hii” Alisema Mhandisi Kuganda.

## IJUE DART



DART
DAR RAPID TRANSIT

# UONGOZI WA DART



**Dr. Edwin Mhede**
*Mtendaji Mkuu*



**Dr. Eliphas Mollel**
*Mkurugenzi wa Utawala, Rasilimali Watu na Mawasiliano*



**CPA. Deusdelity Casmir**
*Mkurugenzi wa Fedha na Maendeleo ya Biashara*



**Dr. Philemon Mzee**
*Kaimu Mkurugenzi Uendeshaji na Usimamizi wa Miundombinu*



**Mha. Fanuel Kalugendo**
*Kaimu Mkurugenzi Maendeleo ya Usafirishaji*



**Domina Madeli**
*Meneja Huduma za Sheria*



**CPA. Flora Fifi**
*Meneja Ukaguzi wa Ndani*



**Ng'wanashigi Gagaga**
*Meneja TEHAMA*



**Scholastica Ndilanha**
*Kaimu Meneja Manunuzi*

# Habari katika Picha



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), Mhe. Jerry Silaa, akisalimiana na maafisa wa DART, alipowasili katika Ofisi za Wakala kwa ajili ya ziara ya Kikazi, Septemba 2022.*



*Baadhi ya wajumbe wa menejimenti ya DART, wakifuatilia hotuba ya Mwenyekiti wa kamati ya Kudumu ya Bunge ya uwekezaji wa mitaji ya Umma (PIC), Mhe. Jerry Silaa, alipofanya ziara ya kikazi. Septemba 2022.*



*Kaimu Mkurugenzi wa Uendeshaji na Usimamizi wa Miundombinu, Dr. Philemon Mzee akifafanua jambo kwa wajumbe wa kamati ya kudumu ya Bunge, ywa Uwekezaji mitaji ya umma (PIC) katika kituo kikuu cha Kimara, Septemba 2022.*




*Aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Raisi - TAMISEMI, Mhe. Innocent Bashungwa (katikati) akiwa na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka, Dr. Edwin Mhede na Mwenyekiti wa PIC, Jerry Silaa, wakiwa kwenye basi la Mwendokasi, wakati kamati hiyo ilipofanya ziara, Septemba 2022.*

# *Habari katika Picha*



*Mhandisi Nebu Kyando akifafanua jambo kwa wajumbe wa Mamlaka ya Barabara za Mijini kutoka nchini Kenya (KURA), walipofanya ziara ya mafunzo katika wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka, Septemba 2022.*



*Mhandisi Nebu Kyando akitoa maelezo ya uendeshaji wa Mabasi, katika moja ya mabasi ya DART kwa wajumbe wa Mamlaka ya Barabara za Mijini kutoka nchini Kenya (KURA), walipofanya ziara ya mafunzo katika wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka, Septemba 2022.*



*Wajumbe wa Mamlaka ya Barabara za Mijini kutoka nchini Kenya (KURA), wakipatiwa maelezo ya mfumo mpya wa ukusaji wa nauli, AFCS, Septemba 2022.*



*Mhandisi, Mohamed Kuganda, akitoa maelezo ya namna ya kutumia programu tumizi ya Dar City Navigator, wajumbe wa Mamlaka ya Barabara za Mijini kutoka nchini Kenya (KURA), Septemba 2022.*

DART
DAR RAPID TRANSIT

# DAR CITY NAVIGATOR APP


## SASA UNAWEZA KUKATA TIKETI YA MABASI YAENDAYO HARAKA KIGANJANI MWAKO.

**Ni rahisi**

1. Ingia Playstore kwa watumiaji wa Android au App Store kwa watumiaji wa IOS.
2. Tafuta program ya 'Dar City Navigator' na uipakue
3. Fungua program na uende kwenye kata tiketi
4. Kisha ingiza namba yako ya simu (hii ni mara moja)
5. Chagua kituo cha kupandia na bidhaa kisha tuma
6. Hakiki taarifa na kisha bofya lipia tiketi
7. Chagua mtandao wa simu utakaolipia tiketi, kisha weka namba ya simu.
   **Airtel Money | HaloPesa | TigoPesa | M-Pesa**
8. Ingiza namba ya siri
9. Bofya kukamilisha
10. Ukiwa kwenye tiketi zangu utaiona tiketi yako

Available on the Google Play

Download on the App Store




## DART HUDUMA KWA WATEJA

Kwa maoni, ushauri na msaada

# 0800 110 147

Muda: 11:00 Alfajiri - 05:00 Usiku

DARTMwendokasi | DART TV | 0800 110 147 | www.dart.go.tz